



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA



27 JULAI 2021

Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb. Na. UDC/L10/10/IV/87

SAID SULAIMAN ABDULLAH AL-SHARJI,  
P. O BOX: 1410 RUWI,  
PC: 112, SULTANATE OF OMAN.

**YAH: MAOMBI YA ENEO LA EKARI 120 KWA AJILI YA UWEKEZAJI KILIMO CHA  
TENDE NA MICHIKICHI.**

Barua yako isiyokuwa na Kumb. Na. ya tarehe 08/06/2021 juu ya mada tajwa hapo juu yahasika,

2. Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, kwa sasa imeanzisha mpango wa kukuza na kuongeza tija katika kilimo cha Michikichi. Ili kufikia lengo hilo, imeanzisha mashamba vitalu ya michikichi yatakayopimwa na kumilikishwa kwa wananchi na wawekezaji wengine wenye nia na uwezo wa kuwekeza katika kilimo cha chikichi. Sambamba na hilo, tumekuwa pia tukipokea wawekezaji wengine katika nyanja za kilimo na mifugo na kuwapatia ardhi kwa. Hali hii imeifanya Halmashauri hii kuwa na mashamba mengi yaliyopimwa na kumilikishwa ikiwa ni pamoja na mashamba yaliyomilikishwa kwa wawekezaji wasio raia wa Tanzania kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).
3. Kama ulivyojieleza kuwa wewe sio raia wa Tanzania, na kwamba unatambua umiliki wa Ardhi Tanzania kwa mtu asiye Raia unawezekana tu pale Ardhi inapotumika kwa ajili ya uwekezaji na kwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania na kwamba unahitaji kupata uhakika wa kupata Ardhi ili ukamilishe taratibu za kuwasilisha maombi yako TIC ikiwa ni pamoja na kujisajili kama mwekezaji kama ulivyoshauriwa. Kwa barua hii, ninakupatia uhakika wa kupata Ardhi katika Wilaya ya Uvinza kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha michikichi katika mashamba vitalu yaliyoandaliwa na kilimo cha mazao mengine katika maeneo mengine yaliyo ndani ya Wilaya.

Jengo la Utawala: Mtaa wa Lugufu, S.L.P 12, Uvinza/Kigoma. Simu No; +255 028 280, Nukushi; No; 028 280.  
Baruapepe: [ded@uvinzadc.go.tz](mailto:ded@uvinzadc.go.tz)/ Tovuti; <http://www.uvinzadc.go.tz>

4. Kwa sababu hiyo, unatakiwa kuwasilisha maombi yako TIC na baada ya ofisi yangu kujiridhisha kuwa umetimiza matakwa na vigezo vyote vinavyotakiwa na na TIC itaendelea na maombi yako ikiwa ni pamoja na kukupatia hati ya madai (invoice) ya malipo stahiki ya umiliki wa ardhi kwa matumizi uliyokusudia.
5. Baada ya kukamilisha malipo, Ardhi hiyo itamilikishwa kwa TIC na wewe utapatiwa Hati Miliki isiyo ya Asili (Derivative Right) toka TIC

Nakutakia utekelezaji mwema.



Manyama Makongo  
Kny: MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**UVINZA**

Mny. MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**UVINZA**

**Nakala:**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri – Aione ndani ya Jalada

